

# HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa KondoA)*

MJI WA KONDOA

Simu: +255 262360028

Fax: +255 262360028

Baruapepe: td@kondoatc.go.tz

Tovuti: www.kondoatc.go.tz



Idara ya Maendeleo ya  
Jamii

Sanduku la Posta 711,  
KONDOA

TAREHE 18/03/2020

## TANGAZO LA MIKOPO KWA VIJANA, WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAVITANGAZIA VIKUNDI **VYA VIJANA, WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU** KUWA, HALMASHAURI IMETENGA FEDHA **ASILIMIA KUMI** YA MAPATO YA NDANI KWA KIPINDI CHA **JANUARI HADI MWEZI MACHI 2020** KWA AJILI YA KUWAPATIA MIKOPO YA KUWAWEZESHA KUENDESHA MIRADI NA BIASHARA ZAO ILI KUJIKWAMUA KIUCHUMI.

VIKUNDI VITAKAVYOOMBA MIKOPO HIYO NI VILE AMBAVYO VIMESAJILIWA NA KUPEWA CHETI CHA USAJILI NA KUWA NA SIFA ZIFUATAZO;

1. KIKUNDI LAZIMA KIWE KINAJISHUGHULISHA NA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI MDOGO AU WA KATI KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA.
2. KIKUNDI KIWE KIMESAJILIWA KAMA KIKUNDI CHA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.
3. KIKUNDI CHA **WANAWAKE NA VIJANA** KIWE NA WANAKIKUNDI KUANZIA **KUMI(10)** NA KUENDELEA NA KIKUNDI CHA WATU **WENYE ULEMAVU** KIWE NA WANAKIKUNDI KUANZIA **WATANO(5)** HADI **KUMI (10)**
4. KIKUNDI KIWE NA AKAUNTI BENKI ILIYO HAI NA ISOMEKE KWA JINA LA KIKUNDI NA KIKUNDI KIAMBATANISHE **TAARIFA YA BENKI (BANK STATEMENT)** KWENYE MAOMBI

5. WAKAKIKUNDI LAZIMA WAWA NI RAIA WA TANZANIA WENYE **AKILI TIMAMU** NA UMRI WA MIAKA **KUMI NA NANE** NA KUENDELEA NA KIKUNDI CHA VIJANA MWISHO UMRI WA **MIAKA 35**.
6. KIKUNDI KISIJUMUISHE WAJUMBE WENYE **AJIRA RASMI**
7. KIKUNDI KIWE NA BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA KWA MTENDAJI WA MTA A HUSIKA.
8. KIKUNDI KINATAKIWA KUJAZA FOMU **MAALUM YA MAOMBI YA MIKOPO** INAYOPATIKANA KATIKA OFISI ZA WATENDAJI WA MITAA NA KUAMBATANISHA NA MAOMBI YAO.

HIVYO VIKUNDI VYOTE VYENYE SIFA HAPO JUU VINATAKIWA KUANDIKA MAOMBI YA KUOMBA MKOPO NA VIKUNDI VILIVYOKWISHAOMBA AWALI VINASHAURIWA KUOMBA TENA.

MUHIMU: VIKUNDI VYOTE VITAKAVYOOMBA MKOPO VITATAKIWA KUANDIKA MCHANGANUO WA BIA SHARA NA BARUA YA MAOMBI KUPITIA KWA **MTENDAJI WA MTA A, NAKALA YA CHETI CHA USAJILI** PAMOJA NA KUAMBATANISHA NA **MUHTASARI WA KIKAO NA MAHUDHURIO**.

MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA ANWANI IFUATAYO

**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI KONDOA  
S.L.P 711  
KONDOA**

MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI **TAREHE 06/04/2020**

LIMETOLEWA NA



MSOLENI DAKAWA

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI  
KONDOA**

